



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MJİ MAFINGA

Unapojobu tafadhali taja:

HM/MAF/S.50/17/79

05 Julai, 2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mafinga anakaribisha maombi ya nafasi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenyе sifa na uwezo wa kujaza nafasi ya **Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II**. Tangazo hili linatokana na kibali cha ajira mbadala kilichotolewa na Katibu Mkuu (UTUMISHI) kwa barua yenye Kumb. Na. FA. 170/363/01/"A"/84 ya tarehe **08 Juni, 2023**.

1.0: MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II – NAFASI 02

1.1: MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kuorodhesha barua zinazoingia masjala kwenye rejista (incoming correspondence register).
- ii. Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya Taasisi kwenye rejista (outgoing correspondence register).
- iii. Kusambaza majalada kwa Watendaji (Action Officers).
- iv. Kupokea majalada yanayorudi masjala kutoka kwa Watendaji.
- v. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/majalada yanayohitajika na Watendaji
- vi. Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada (racks/filling cabinets) au mahali pengine yanapohifadhiwa.
- vii. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi (File tracking).
- viii. Kufungua na kuweka barua au nyaraka kwenye majalada.

2.0: SIFA ZA MWOMBAJI

Awe na cheti cha kuhitimu elimu ya kidato cha nne au kidato cha Sita mwenye Stashahada au NTA level Six katika fani mojawapo kati ya zifuatazo;- Utunzaji wa Kumbukumbu, Urasimu Ramani (Cartography) au (Geoinfomatics), Sheria, au Kumbukumbu za Afya kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali, awe na ujuzi wa kompyuta.

0: MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya Serikali yaani **TGS C.**

4.0: MASHARTI YA JUMLA.

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenyewe umri usiozidi miaka 45.
- ii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa, nakala ya kitambulisho cha Taifa au namba ya kitambulisho cha Taifa.
- iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- v. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma na vyeti vya elimu (nakala za vyeti zithibitishwe na Wakili/Mwanasheria/Hakimu)
- vi. Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (**Form IV and Form VI Results Slips**) **Havitakubaliwa.**
- vii. Waombaji waambatanishe picha mbili (passport size) za hivi karibuni
- viii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).
- ix. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- x. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **Hayatafikiriwa.**
- xi. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **18 Julai, 2023.**

Muhimu: Maombi ya nafasi hii yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi wa Mji,
Halmashauri ya Mji Mafinga,
S.L.P 76,
MAFINGA.

Limetolewa na;

Ayoub J. Kambi
MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI MAFINGA

